

Please check the examination details below before entering your candidate information

Candidate surname					Other names				
Centre Number					Candidate Number				

Pearson Edexcel International GCSE (9–1)

Thursday 29 May 2025

Afternoon (Time: 2 hours 15 minutes) **Paper reference** **4SW1/01**

Swahili

PAPER 1: Reading, Writing and Translation

You do not need any other materials.

Total Marks

Instructions

- Use **black** ink or ball-point pen.
- **Fill in the boxes** at the top of this page with your name, centre number and candidate number.
- There are **three** sections you must answer:
 - Section A Questions 1–4
 - Section B Questions 5 and **either** Question 6(a) **or** 6(b) **or** 6(c)
 - Section C Question 7.
- Answer the questions in the spaces provided
 - *there may be more space than you need.*
- You must **not** use a dictionary.

Information

- The total mark for this paper is 80.
- The marks for **each** question are shown in brackets
 - *use this as a guide as to how much time to spend on each question.*

Advice

- Read each question carefully before you start to answer it.
- Check your answers if you have time at the end.

Turn over ►

P79742A

©2025 Pearson Education Ltd.
Y:1/1




Pearson

SECTION A

Reading

Answer ALL questions.

Write your answers in the spaces provided.

Multiple-choice questions must be answered with a cross in a box ☐. If you change your mind about an answer, put a line through the box ☒ and then mark your new answer with a cross ☐. Open-response questions do not have to be written in full sentences and you may respond using single words or phrases.

- 1 Malizia sentensi zifuatazo kwa **Kiswahili** na tumia taarifa katika maelezo. Weka alama sahihi kwenye kila kisanduku.

Chapati

Chakula cha jioni katika familia nyingi kisiwani Zanzibar na sehemu nyingi duniani ni chapati. Watu hula chapati pamoja na mchuzi wa kuku wa kienyeji, ingawa chapati na maharagwe ya nazi ni maarufu zaidi.

Mapishi ya chapati si rahisi kwani yana hatua nyingi. Inabidi kuchanganya unga, chumvi na maji ingawa utamu hasa wa chapati hutokana na samli. Zamani watu walikanda na kusukuma chapati kwa mikono. Siku hizi wengi hutumia mashine kwani ni haraka zaidi na wapishi hawataki kuchoka. Muundo wa jadi wa chapati ni duara ingawa siku hizi wengine hupendelea chapati mraba. Migahawa midogo inapendelea kuuza chapati kwani ni nadra kuzipika majumbani.

- | | | | |
|-------------------|----------------|-----------------------|--------------------|
| A mraba | B kuku | C upesi | D mchezo |
| E biashara | F ladha | G wanaruhusiwa | H ghali |
| I duara | J hatua | K jioni | L maharagwe |
| M harufu | | | |

Example:	Chapati huliwa wakati wa ...	K
1 (a)	Watu hupendelea zaidi kula chapati na ...	
1 (b)	Ugumu wa mapishi ya chapati hutokana na wingi wa ...	
1 (c)	Samli huipa chapati ... bora	
1 (d)	Mashine husaidia kukanda kuwa ...	
1 (e)	Muundo wa sasa wa chapati ni ...	
1 (f)	Mapishi ya chapati yamekuwa ...	

(Total for Question 1 = 6 marks)



DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

BLANK PAGE



- 2 Weka alama katika visanduku **10** vilivyo sahihi. Sentensi nyingine au watu wengine wanaweza kuwa na alama zaidi ya moja au bila alama yoyote.

Kusoma nchi tofauti

Asha




Nilipata nafasi ya kwenda kusoma katika shule tofauti nchini Kenya. Mwenyeji wangu alikuwa msichana mzuri. Familia yake ilinikaribisha kwao na nilienda kusoma shuleni kwake. Niliweza kujifunza lugha mpya ya Kiswahili na pia kutembelea makumbusho tofauti. Nilipenda kuwa nchini huko na nikaamua kurudi na kufundisha Kiingereza baadaye.

Sabrina



Chuo changu hakina mfumo wa kuwawezesha wanafunzi kusoma nchi tofauti. Inasikitisha. Wakati ujao nitapenda kuwa mfasiri, kwa hivyo nimeamua kuwasiliana na mwenyeji nchini Tanzania kujifunza lugha. Kuna mvulana ambaye amekubali kunialika kwao na nitaenda kukaa mwezi mmoja hivi karibuni.

Hirsi



Mara ya mwisho nilipoenda kusoma nchi tofauti nilikaa mwezi mzima. Nilipokuwa huko sikuenda katika matembezi yoyote ya kitamaduni. Nilibaki katika nyumba ya familia ya mwenyeji wangu muda wote. Kwa bahati mbaya, hivi sasa sina mawasiliano na mwenyeji wangu tena.

		Asha	Sabrina	Hirsi
Mfano:	alitembelea Kenya	☒	☐	☐
A	amewahi kuenda kusoma nchi nyingine	☐	☐	☐
B	alisafiri kwa mwezi mmoja	☐	☐	☐
C	alifanya shughuli ya kitamaduni	☐	☐	☐
D	ameshakutana na mwenyeji wake	☐	☐	☐
E	anataka kufanya kazi na lugha	☐	☐	☐
F	amefanya mpango wa kusoma kwingine	☐	☐	☐
G	amepoteza mawasialiano na mwenyeji	☐	☐	☐

(Total for Question 2 = 10 marks)

- 3 Soma makala kuhusu Kujitegemea. Malizia taarifa kwa kutumia namba au maneno kwa **Kiswahili**.

Kujitegemea

Ninaitwa Maria, sasa ni miezi mitatu tangu mimi na rafiki yangu Lela turudi nyumbani kutoka chuo kikuu huku tukiwa tumeshika shahada zetu mkononi. Walakini, hadi sasa bado hatujapata kazi ya maana, kwa hivyo hatuna pesa za kutosha ili kujitegemea.

Wiki iliyopita nilipata nafasi ya kufundisha somo la hisabati katika shule moja karibu na kijiji walichozaliwa wazazi wangu. Mwalimu wao wa kawaida aliumwa hivyo Mwalimu mkuu alinitafuta. Alipata namba yangu ya simu kwenye maombi niliyotuma shuleni hapo ili kuomba kazi. Awali niliogopa lakini baadaye nilifurahia na ninategemea wataniajiri.

Kwa upande mwingine, Lela anapenda kulala siku nzima na hajafanya juhudi zozote kupata ajira. Ili kumsaidia kupata pesa, nimemshauri aoshe magari mtaani kwake ili wenyewe waonekane maridadi wanapokwenda kanisani Jumapili. Pia angeweza kutembeza mbwa jioni. Nimemshauri atangaze huduma hizi mtandaoni na kubandika matangazo mtaani.



Mfano: Muda tangu kurudi nyumbani: **Miezi mitatu**

(a) Pingamizi katika kujitegemea: na
..... (2)

(b) Ajira aliyopata Maria: (1)

(c) Sehemu wanapotoka wazazi wa Maria: (1)

(d) Sababu ya mwalimu kutofundisha: (1)

(e) Hisia za Maria kuhusu kazi: na
..... (2)

(f) Shughuli ya Lela kila siku: (1)

(g) Sababu ya kutaka gari safi: (1)

(h) Muda wa kutembeza mbwa: (1)

(i) Jinsi ya kutangaza huduma: na
..... (2)

(Total for Question 3 = 12 marks)

- 4 Soma habari ifuatayo kutoka kitabu kiitwacho **Kasri ya Mwinyi Fuad**, kilichoandikwa na Shafi Adam Shafi.

Kijakazi

Huku jasho likimtirikika Kijakazi aliendelea na kazi zake tangu asubuhi hadi magharibi.

Usiku aliingia chumbani mwake na kujinyoosha kitandani huku macho yake yakiangalia dari. Dari lake lilikuwa na mbao za boriti zenye rangi kahawia. Zilikuwa sambamba, moja baada ya nyingine. Chumbani kwake kulikuwa na shanga alizoweka ukutani na zilizoonekana kutokana na mwanga wa taa ya kibatari iliyokuwa mezani na iliyotoa mwangaza mdogo uliomwezesha kuona hali yake duni ya maisha.

Mwanga haukuweza kumwonyesha jinsi ya kujikomboa. Chumba chake hakikuwa na sakafu bali udongo alioumwagia maji ili kupunguza vumbi na kwenye mlango palitundikwa gauni lake bovu bovu la kijivu alilolivaa kila siku.

Mara mazungumzo yake na rafiki yake, Mkongwe, yalimjia akilini na akafumba macho na kujitahidi kuitoa kumbukumbu hiyo kwa kutingisha kichwa. Lakini mazungumzo yake na Mkongwe yalimjia tena,

‘kwa nini unakubali kufanya kazi kama punda?’ Mkongwe alimwuliza

‘mimi sijali pesa shoga yangu, ninajali utiifu kazini’ Kijakazi alijibu

‘unapoteza maisha yako. Sasa mapinduzi yanakuja na hatupaswi kuogopa tena!’ alisema Mkongwe.

Kijakazi aliduwaa huku akimwalia Mkongwe na kusema ‘una maana gani?’

Jibu maswali kwa **Kiswahili** na tumia taarifa katika maelezo. Si lazima kuandika sentensi kamili.

- (a) Tunajuaje kwamba Kijakazi alifanya kazi nzito?

Taja maelezo **mawili**.

(2)

- (b) Taja maelezo **mawili** kuhusu paa la chumba cha Kijakazi.

(2)



(c) Taja maelezo **mawili** kuhusu sakafu ya chumba cha Kijakazi.

(2)

(d) Matendo gani yanaonyesha Kijakazi hafurahii kumbukumbu ya Mkongwe?

Taja maelezo **mawili**.

(2)

(e) Kijakazi anahisi wajibu wake kazini ni nini?

(1)

(f) Tunajuaje kwamba Kijakazi hakuwa tayari kwa mapinduzi?

(1)

(Total for Question 4 = 10 marks)

TOTAL FOR SECTION A = 38 MARKS



P 7 9 7 4 2 A 0 9 1 6

SECTION B

Writing

Answer Questions 5 and either Question 6(a) or 6(b) or 6(c).

Write your answers in the spaces provided.

5

Michezo

Mchezo uliocheza
karibuni

Umuhimu wa
michezo

Mwanamichezo
mashuhuri nchini kwako

Mchezo mpya
utakaocheza siku zijazo

Andika takriban maneno 70 kwa **Kiswahili** kuhusu mchezo. Ni lazima kutumia maneno yote yaliyotajwa hapo juu.

(12)

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA



DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

Handwriting practice area with 24 horizontal dotted lines.

(Total for Question 5 = 12 marks)



- 6 Chagua **moja** kati ya maswali matatu yafuatayo na andika takriban maneno 130 kwa **Kiswahili**.

Chaguo 1



- (a) Andika hotuba kuhusu ajira za kujitolea. Ni lazima uandike kuhusu:

- Kwa nini vijana wafanye kazi za kujitolea
- Ajira ya kujitolea uliyoifanya
- Shirika utakalopenda kufanyia kazi za kujitolea baadaye.

(20)

Chaguo 2

- (b) *Mpendwa Hannah*

Baada ya kufanya kazi zangu za nyumbani leo niliamua kukuandikia barua pepe hii ili kukuuliza jinsi unavyosaidia kazi nyumbani kwenu.

Rafikiyo,

Aaliyah

Jibu kwa kutumia barua pepe. Ni lazima uandike kuhusu:

- Ulisaidiaje nyumbani jana
- Kwa nini vijana wasaidie nyumbani
- Mtu unayetaka kumsaidia kazi za nyumbani baadaye.

(20)

Chaguo 3

- (c) Kwenye ukurasa wako wa blogu andika kuhusu jamii yako. Ni lazima uandike kuhusu:

- Shughuli mnazofanya kwa pamoja
- Tukio ambalo ungetaka jamii ifanye mwaka ujao
- Mtu wa zamani ambaye ni muhimu katika jamii yako.

(20)



DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

(Total for Question 6 = 20 marks)

TOTAL FOR SECTION B = 32 MARKS



SECTION C**Translation into Swahili****Write your answer in the space provided.****7** Tafsiri aya ifuatayo kwa **Kiswahili**.**Winning a competition**

Two brothers from Tanzania have won a reality competition. They were able to beat nine other finalists. In the final show, one of them climbed up and down a long ladder, while carrying the other one on his head. The audience found the show terrifying and clapped loudly.

These young men have said that they want to use the prize money to help other acrobats, by building a new training centre in their town. They will also buy more equipment and pay trainers to go into schools.

(Total for Question 7 = 10 marks)**TOTAL FOR SECTION C = 10 MARKS
TOTAL FOR PAPER = 80 MARKS**

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

BLANK PAGE

Source Information

Question 2

- © skyNext/Getty Images
- © SDI Productions/Getty Images
- © Getty Images

Question 6

- © PeopleImages/Getty Images

